

JUZUU 1

WATOTO



PLAY KIT

YA KUJIFUNZA

SETI YA KUCHEZA NA KUJIFUNZA NYUMBANI NA SHULENI

WACHA TUANZE

Jedwali La Yaliyomo

Michezo Kumi ya Kucheza

1. Namba ya mti wa mwembe
2. Kugusa na kuhisi
3. Pindua blanketi
4. Anzisha duka lako mwenyewe
5. Kujenga daraja
6. Kuhusu ulimwengu wangu
7. Kwa nini matunda yanageuka kahawia (brown)
8. Taa ya lava
9. Ramani ya jirani
10. Maji ya kutembea

1

Habari,

Karibu kwenye seti yetu mpya ya kucheza. Tumefurahi sana kukutana nawe. Tumekutengezea michezo kumi ya kusisimua ili ucheze peke Yako na marafiki au familia.

Umefurahia? Haya ni baadhi ya vidokezo



2

Upande wetu wa kushoto ni jedwali yaliyomo na orodha ya michezo unayoweza kucheza.

Upande wa kulia tuna wanyama kumi wa kupakwa rangi. Unaweza kupaka rangi Kila myama ,ukishamaliza kucheza Kila mchezo. Kila mnyama ana nambari karibu naye ili uweze kujua ni mnyama yupi wa kutia rangi mwishoni mwa kila mchezo.




3

Pia utaweza kupata beji mbili za kupendeza, Moja unapomaliza michezo mitano ya kwanza na beji ya pili baada ya kumaliza michezo yote kumi.








4

Umeelewa Kila kitu?
Tuanze mchezo!



Wapake Rangi Wanyama




VIFAA:

Karatasi, Kete Mbili (Dice)

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Hesabu

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Dakika 30




1

Chora mti kwenye kipande cha karatasi




2

Tengeneza matawi ya mti na uyaandike nambari 2 Hadi 12



3

Kwenye karatasi nyingine chora na ukate maembe kumi na mawili. Hizi zitatumika kufunika nambari



4

Tembeza kete. Ongeza nambari 2 na ufunike TAWI la mti yanayofanana, kwa mfano, ukikunja 3 na 4, funika TAWI la nambari 7



5

Tembeza kete. Hadi matawi yote ya mti yafunikwe




Matokeo ya Mwisho

MCHEZO : Mwembe wa Nambari

Paka rangi kwa mwembe na utumie kucheza mchezo.


Kata maembe na utumie kama ilivyoagizwa.




Maembe



KIOLEZO CHA SHUGHULI NA RASILIMALI



KIOLEZO CHA SHUGHULI NA RASILIMALI




VIFAA:

Boksi la Kadibodi, Makasi, Vitu Tofauti


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Mazingira


MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Dakika 30



Kata shimo kubwa kwenye kisanduku, hakikisha mkono wako umetoshea ndani



2

Weka kitu kwenye kisanduku lakini usiwambie mtu yeyote ulichoweka ndani. Kwa mfano unaweza KUWEKA mahindi, tufaha, mmea au mswaki na kadhalika



3

Mwambie mtu mwingine aweke mkono wake ndani ya kisanduku na kusema nini kilichopo ndani. Je, ni ngumu au laini? Je ni umbo gani?



**Matokeo
ya Mwisho**


VIFAA:

Shuka Ya Kitanda, Gazeti Au Blanketi


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Dakika 30



1 Weka/Tandika Shuka chini



2 Watoto wawili au watatu wanaweza kusimama juu ya Shuka, gazeti au blanketi



3 Timu lazima ishirikiane kugeuza Shuka bila hata Moja wenu kukanyaga chini sakafuni



4 Ikiwa mtu yeyote atagusa chini kwa sakafu, lazima uanze tena

Matokeo ya Mwisho



VIFAA:

(Makopo, Chupa) Tupu za Chakula, Pesa za Kirongo za Karatasi

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Lugha na Kusoma (Kiingereza au Kiswahili)

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Saa 1




1

Chagua watoto tofauti na uwape majukumu tofauti katika duka. Kwa mfano: muuzaji, mtunza fedha na askari wa kulinda



2

Panga vitu vyote kwenye meza. Unaweza kuweka chupa tupu za chakula, sabuni au nguo. Weka bei kwenye kila kitu



3

Hakikisha umetengeneza pesa za makaratasi



4

Kila mtu achukue nafasi yake dukani. Wanunuzi waingie dukani na kuchagua vitu ambavyo wanataka kununua na kuchukua kwa cashier kulipa. Kuwa na mazungumzo na kila mmoja. Kwa mfano wanunuzi wanafananisha bei na kuuliza muuzaji kama kuna mali mapya imeingia au kuna offer spesheli






5

Muuzaji anafanye hesabu na kufunga vitu pamoja mnunuzi analipia vitu




Matokeo ya Mwisho

MCHEZO : Anzisha Duka Lako Mwenyewe
Tengeneza nakala za pesa za mchezo na utumie kucheza
'Anzisha Duka Lako Mwenyewe'



MCHEZO : Anzisha Duka Lako Mwenyewe
Tengeneza nakala, weka rangi na ukate lebo za bei za kutumia kwenye mchezo




VIFAA:

Magazeti, Gari la Kirongo, Ukanda, Kamba, Gundi, Uzi

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sayansi na Teknolojia

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Dakika 30



1 Tengeza daraja la karatasi ukitumia gazeti. Unaweza kuisokota, kuikunja na kutandaza karatasi




2 Jaribu kuunda daraja la karatasi ambalo lina nguvu ya kutosha ili kigari kivuke bila kuvunjika



3 Jaribu kuvukisha gari kwenye daraja la gazeti. Na useme "wasee wasee", na ujibu na "msee, msee". Dereva atasema "nataka kuvuka ng'ambo ile lakini daraja kaporomoka". Kisha itikia kwa kumwambia dereva aseme maneno ya ajabu na daraja litajengwa tena.

Matokeo ya Mwisho



VIFAA:

Magazeti, (Magazines) na Makasi

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Ubunifu ya Sanaa, Mienendo

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Saa 1




1

Kwa magazeti/ (magazines) tafuta picha na maneno kuuhusu wewe mwenyewe



2

Kata picha na uunganishe kwa gundi kwenye karatasi



3

Kuwa mbunifu, waweza kuchanganya vitu unavyopenda kama, kula na kufurahia kwa mfano kula chokoleti, keki ama kucheza mpira wa miguu





4


Waonyeshe picha yako marafiki zako



Matokeo ya Mwisho



GAME : Kuhusu Dunia Yangu
Tengeneza nakala na ukate vitu unavyovipenda ikiwa huwezi kupata picha yako mwenyewe




VIFAA:


Ndizi, Kisu, Limau

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sayansi na Teknolojia

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:

Dakika 30



1

Kata ndizi na ukate limau



3

Wacha kwa dakika kumi.
Unadhani ndizi gani itabadilika
kuwa kahawia (brown)



5

Kula ndizi

2

Kwenye sahani moja weka kipande
cha ndizi. Kwenye sahani nyengine
weka kipande cha ndizi na uikamulie
maji ya limau juu



4

Kipande cha ndizi kilicho na maji ya limau
hakikubadilika kuwa kahawia kwa sababu
maji ya limau huzuia hewa safi ambayo ni
oksijeni kuchanganyika na kipande hicho cha
ndizi, hivyo kuzuia oksidishaji(oxidation)

**Matokeo ya Mwisho**


VIFAA:

Chupa ya Maji ya Plastiki, Mafuta ya Kupikia, Rangi ya Chakula, Soda ya Kuokea (Baking Soda)

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sayansi na Teknolojia

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Dakika 30

1



Weka maji nusu chupa

2



Ongeza matone ya rangi ya chakula

3



Jaza mafuta ya kupikia katika sehemu ilobakia kwenye chupa

4



Weka soda ya kuokea (baking soda) kidogo ndani ya chupa. Angalia maji yakichemka na kupeleka mapovu ya maji ya rangi kupitia kwenye mafuta.



Matokeo ya Mwisho

VIFAA:

Kalamu, Penseli, Kalamu za Alama (Marker Pens), Karatasi, Rula

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:




Saa 1



1


Je, ramani iko na taarifa gani? Inaweza kuwa na shule yako, nyumba yako, mahali unaponunua matunda na mboga, kanisa/msikiti n.k.



2

Chora ramani ya pahali unapoishi. Jumuisha (weka pamoja na) maduka, nyumba ya jirani yako, nyumba ya rafiki yako bora, shule na mahali pa maombi.

Matokeo ya Mwisho



MCHEZO : Ramani ya Kitongoji

Tumia lebo hizi kuashiria mahali ambapo maeneo haya yako kwenye ramani yako.

NYUMBANI

STENDI YA MATUNDA/MBOGA

MAHALI PANGU PA KUSALI

NYUMBA YA JIRANI YANGU

SHULE

VIFAA:

Glasi Inayoonyesha (Clear Glass),
Maji, Kitambaa, Rangi za Chakula.

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sayansi na Teknolojia

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Saa 1



1

Jaza maji kwenye glasi 4 zinazoonyesha. Jaza kukaribia juu kabisa.



2

Ongeza tone moja la rangi nyekundu ya chakula kwenye glasi 2, tone moja ya rangi ya samawati kwenye glasi moja na tone moja ya rangi ya manjano ndani ya glasi moja.



3

Panga glasi kwa mstari na glasi iliyo tupu iwe kati ya kila glasi yenye maji ya rangi.



4

Kunja vitambaa 6 na uunganishe na glasi.



5

Maji na rangi itaanza kusonga juu.



Matokeo ya Mwisho

**SHUGHULI
ZA MICHEZO
BEJI ZA MCHEZO
»»**

HONGERA!

Kwa kupata beji yako ya kwanza

BEJI: Ninapata kusoma kwa dakika 30 na mama au baba yangu

Kata na uvae mojawapo ya beji hizi za michezo kwa kujivunia



OR



HONGERA!

Kwa kupata beji yako ya pili

BEJI: Ninapata kuunda mchezo mpya wa kucheza na wazazi

Kata na uvae mojawapo ya beji hizi za michezo kwa kujivunia





JUZUU 1
WATOTO



JUZUU 2
PAMOJA NA WATOTO

PLAY KIT
YA KUJIFUNZA

SETI YA KUCHEZA NA KUJIFUNZA NYUMBANI NA SHULENI